


## Mafundisho ya Kristo

Mafundisho ya Yesu Kristo katika Bibilia yamekuwa kwa muda mrefu upizio kwa wanadamu. Kuna mafundisho zaidi ya mwokozi katika kitabu cha maandiko matakatifu—Kitabu cha Momoni: Ushuhuda Mwingine wa Yesu Kristo. Vitakuletea amani ya kudumu na furaha kwa kukupatia mwongozo wu upuzio katika maisha yako.

Ili ujipatie nakili ya bure ya Kitabu cha Momoni: Ushuhuda Mwingine wa Yesu Kristo, piga simu kwa nambari hii 1-800483-1800.

KANISA LA
YESU KRISTO
LA WATAKATIFU
WA SIKU ZA MWISHO

© 1998 by Intellectual Reserve, Inc.
Haki zote zimehifadhiwa
Kimechapishwa katika United States of America
Kingereza kiliidhinishwa: 9/99
Tafsiri Iliidhinishwa: 9/99
Tafsiri ya *The Testimony of the Prophet Joseph Smith*
Kiswahili
SWAHILI
32667 743

# Ushuhuda wa Nabii Joseph Smith

Kanisa la Yesu Kristo
la Watakatifu wa Siku
za Mwisho



## Joseph Smith: Nabii wa Mungu

*Wakati Joseph Smith alipokuwa na miaka 14, alitaka kujua ni kanisa gani ambalo angejiunga nalo, kwa hivyo alimuuliza Mungu katika maombi ya kikweli. Katika majibu kwa maombi haya, Mungu Baba na Mwanawe, Yesu Kristo, walimtokea Joseph na kumuambia kwamba kanisa la kweli la Yesu Kristo halikuwepo katika dunia na wamemc hagua Joseph kulirudisha.*

*Kutoka siku hiyo, Joseph alifanya kazi ya Mungu, akifanya kazi ya kulianzisha Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho na kujenga ufalme wa Mungu duniani katika siku za mwisho. Washiriki waaminifu wa kanisa hushuhudia kwamba Yesu Kristo ndiye Mwokozi na Mkombozi wa ulimwengu. Yesu huendesha kanisa lake siku hizi kupitia kwa kumfunulia nabii katika dunia. Joseph Smith alikuwa mmojawapo wa nabii kama hao. Ijapokuwa Joseph alitimiza mambo mengi katika maisha yake, kilichokuwa muhimu zaidi kilikuwa utenzi wa kuwa mfuasi na shahidi wa Yesu Kristo. Aliandika, "Baada ya Ushuhuda mwingi ambao umepeanwa juu yake, huu ni ushuhuda wa mwisho, ambao tunatoa juu yake: Kwamba anaishi!" (Mafuudisho na Maagano [Doctrine and Covenants] 76:22).*

*Wale wanaoupokea ushuhuda wa Nabii kwa nguvu za Roho Mtakatatifu watajua ukweli wa kazi aliyoitwa kufunya. Pia watajua amani na furaha ambayo inayotoka kupitia kwa Mwokozi Yesu Kristo, ambaye Joseph Smith alimwabudu na kumutumikia.*



*Ukiwa katika hali ya kuamua ni Kanisa gani utakalojiunga nalo, Joseph alitafuta maongozi kutoka kwenye Bibilia, hapo alisoma "Muulize Mungu."*

## Ni Kanisa Lipi Lililo la Kweli?

*Joseph Smith alizaliwa mwaka wa 1805 katika Sharon, Vermont. Wakati masimulizi haya yanapoanza, alikuwa na miaka 14, akiishi na familia yake huko New York, na akifikiria kwa dhati ni kanisa lipi angelijiunga nalo. Ufuatao ni uzoeru wa Joseph, ulioandikwa kwa maneno yake mwenyewe.*

Katika wakati huu wa msisimko mkuu, akili zangu ziliitwa kufikiria kwa tahadhari kuu. . . . mara nyinyi nilijiambia: Nini kina-chohitajika kufanywa? Ni nani kati ya Vikundi hi aliye wa kweli; au vyote vimepotoka? Ikiwa mmoja wao alikuwa wa kweli, ni nani na ningejua kwa namna gani?

Wakati nikuwa nikifadhaika kutokana na mashaka yaliyoletwa na mabishano ya vikundi vya watu wa dini, siku moja nilikuwa nikisoma waraka wa Yakobo, sura ya kwanza na mstari wa tano unaosema hivi: "Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote kwa ukarimu, wala hakemei na atapewa."

Sijapata fungu la maneno ya maandiko matakatifu kiningia kwa nguvu zaidi kwenye moyo wangu kama haya yalivyoiniingia wakati huu. Yaliwezenekana kuingia kwa

nguvu kuu katika hisia zote za moyo wangu. Nilifikiria tena na tena, nikijua kama kuna mtu aliyehitaji hekima kutoka kwa Mungu, alikuwa ni mimi; vile ningetenda sikujua na nisingepata hekima zaidi ya ile niliyokuwa nayo wakati huu, nisingelijua; kwa vile waalimu wa dini wa Madhehebu tofauti walielewa fungu la maneno ya maandiko matakatifu hilo kwa njia tofauti hata kuharibu matumaini ya kusuluhisha swala hilo kwa kukimbilia Bibilia.

Baadaye nilifikia uamuzi kwamba ni lazima nikae kwenye giza na kuchanganyikiwa, au sivyo ni lazima nifanye kama vile Yakobo alivyosema, hivyo ni, kumuuliza Mungu. Baadaye nilikata shauri "Kumuuliza Mungu," kwa Sababu nilijua kwamba ikiwa aliwapatia hekima wale waliopungukiwa, na atawapatia kwa ukarimu, na hatawakemea, nitajaribu.

## Ono la Kwanza la Joseph Smith

Na Katika kulingana na hayo, uamuzi wangu wa kumuuliza Mungu, nilienda kichakani Kufanya jaribio. Ilikuwa ni asubuhi njema, siku iliyong'aa, mapema katika musimu wa "Spring" wa mwaka elfu moja mia nane na ishirini. Ilikuwa mara ya kwanza katika maisha yangu nilipofanya jaribio kama hilo, kwa katikati ya kufadhaika kwangu nilikuwa Sijajaribu Kuomba kwa Sauti.



*Mmoja wao aliniambia, Mimi, akiniita Mimi kwa Jina na kusema akimuota yule Mwingine— "Huyu ni Mwanangu Mpendwa Msikize!"*

Baada ya kufika mahali ambapo nilikuwa nimepanga kwenda, baada ya kuangalia na kuona nilikuwa peke yangu, nilipiga magoti na kuanza kumwambia Mungu tashi wa moyo wangu. Hata nilikuwa sijamaliza kufanya hivyo, wakati kwa ghafula nilikamatwa na nguvu fulani ambazo zilinishinda mimi kabisa na zilikwa na uwezo mkuu juu yangu hata kunifunga ulimi mpaka nikashindwa kusema. Giza jingi lilinizingira, na ikaonekana kwangu kwa muda kama vile nilikuwa nimeangamia kwenye uangamizo wa ghafula.

Lakini, nikitumia nguvu zangu zote na kumwita Mungu ili anitoe kutoka kwa uwezo wa huyu adui ambaye alikuwa amenikamata mimi na katika dakika hiyo ambayo nilikuwa tayari kuanguka kukata tamaa na kujiachalia kwenye maangamizo—. Siyo maangamizo ya kimafikira lakini ni kutokana na nguvu za kiumbe fulani kutoka ulimwengu usioonekana, ambacho kilikuwa na nguvu za ajabu ambazo nilikuwa sijawahi kuzisikia hapo mapema katika kiumbe chochote— Saa hiyo ya mshituko huu mkuu, niliona mhimili wa mwangaza hasa juu kichwa changu, uloangaza zaidi ya jua, ambao uliteremka taratibu mpaka ukaanguka juu yangu.

Ulipotokea hivi nilijipata kuwa huru kutokana na adui ambaye amenikamata. Wakati mwangaza ulipotua juu yangu niliona watu wawili, ambao wangavu na utukufu wao



ulishinda maelezo yo yote, Wakisimama juu yangu kwenye hewa. *Mmoja wao aliniambia mimi, akiniita mimi kwa jina na kusema, akimuota yule mwingine— "Huyu ni Mwanangu Mpendwa, Msikize!"*

Shabaha yangu ya kuenda kuuliza kutoka kwa Mungu ilikuwa ni kujua katika madhehebu yote ni lipi lililokuwa la kweli, ili kwamba ningelijua ni lipi nitajiunga nalo. Punde, nilipopata fahamu, niliweza kusema, nikauliza hao watu waliosimama juu yangu katika mwangaza, ni dhehebu gani lililokuwa la kweli (kwa kuwa wakati huu wote ilikuwa haijanijia moyoni mwangu kwamba yote yalikuwa mapotovu)— na ni lipi ambalo linafaa kujiunga nalo.

Nilijibiwa kwamba nisijiunge na lolote kati ya hayo kwa vile yote yalikuwa yenye upotovu; na mtu aliyekuwa akiniongelesha alisema kwamba kanuni za imani zao zilikuwa machukizo machoni mwake; na wale waamini wote walikuwa wapotovu; kwamba: "Kwa kuwa watu hawa hunikaribia na kuniheshimu kwa vinywa vyao, bali mioyo yao wamefarakana nami, na wanafundisha kama kanuni amri za wanadamu, wakiwa na mfano wa Mungu, lakini walikana nguvu zake."

Naye tena akanikataza mimi kijiunga na yoyote kati yao; na mambo mengi aliniambia mimi ambayo siwezi kuandika katika wakati huu. Nilipojifahamu tena, nilijipata nimelala chali, nikitazama mbinguni. Wakati mwangaza ulipotoweka, nilikuwa sina nguvu; lakini punde nilipata nafuu kiasicha kuenda nyumbani.

## Udhalimu

*Joseph alimtii Mungu na hakujiunga na kanisa lolote wakati huo. Na alipowambia watu alichokuwa ameona na kusikia, alianza kukabiliana na ubishi na udhalimu.*

Niligundua. . . kwamba usimulizi wa tokeo hilo ulisababisha uhasini mkuu dhidi yangu kati ya waamini wa dini na kikawa chanzo cha udhalimu mkuu ulioendelea kuongezeka; na kwa vile nilikuwa kijana mnyonge, wa miaka kati ya kumi na nne na kumi na tano, na hali yangu ya maisha kuwa kama vile ilivyo kwa kijana asiye na umaarufu katika ulimwengu, walakini watu maarufu walinitambua hata kuamusha akili za uma dhidi yangu na kuanzisha udhalimu mkali; na hii ilikuwu kawaida katika madhehebu yote— yote yakaungana kunidhalimu mimi.

Lilinifanya mimi kufikiria sana hapo na kila mara kutoka wakati huo, vile jinsi isivyo kawaida kwa kijana asiyejulikana, wa kiasi cha karibu miaka kumi na nne na ambaye alilaz-

imika kupata mahitaji yake ya udhaifu kutokana na kazi ya mikono yake kila siku, angefikiriwa kuwa na umuhimu wa kutosha kushughulikiwa na watu wakuu wa madhehebu mengi mashuhuri ya wakati huo na kwa namna hii hata kufanyika kwao kuwa na moyo wa udhalimu mkali mno na ufidhuli. Lakini ajabu au la, ilikuwa hivyo na ilikuwa mara nyingi chanzo cha huzuni mkuu kwangu.

Walakini, hata hivyo jambo lilikuwa kwamba niliona ono. Nimefikiria kutoka wakati huo, kwamba nikasikia hasa kama Paulo, wakati alipojitetea mbele za Mfalme Agripa na kueleza juu ya tokeo la ono alilokuwa amepata wakati aliona mwangaza na kusikia sauti; lakini bado kulikuwa tuu na wachache ambao walimuamini, wengine walisema kuwa alikuwa mwongo, wengine walisema kuwa alikuwa mwenda wazimu; na alipuuzwa na kushutumiwa. Lakini haya yote hayakubadilisha uhakika wa ono lake. Alikuwa ameona ono, alijua amepata kuona, na udhalimu wowote chini ya mbingu haungeweza kuleta mageuzi yoyote; na hata kama wangemudhalimu yeye hata kifo, bado alijua na atajua mpaka pumzi zake za mwisho, kwamba alikuwa ameona mwangaza na kusikia sauti ikizumgumza naye, na ulimwengu wote hauwezi kumfanya kufikiria au kuamini vingine.

Na hivyo ndivyo ilivyokuwa. Nilikuwa hasa nimeona mwangaza na kati ya huu mwangaza niliona Watu wawili na kwa hakika waliongea nami; na hata kama nilikuwa nimechukiwa na kudhalimiwa kwa kusema kwamba nilikuwa nimeona ono, ila ilikuwa ni kweli; na walipokuwa wakinidhalimu mimi, kunishutumu mimi na kuongea kila aina ya uovu juu yangu kwa uwongo kwa kusema moyo, nilielekezwa kusema katika moyo wangu: kwa nini munidhalimu kwa kusema ukweli? Nilikuwa kwa hakika nimeona ono; na mimi ni nani kushindana na Mungu, au kwa nini ulimwengu ulifikiria kunifanya nikane kile ambacho kwa hakika nilikuwa nimeona? Kwa vile *nilikuwa nimeona ono; nilijua hivyo, na nilijua kwamba Mungu alijua hivyo na singeweza kukana hivyo, na kudhubutu kufanya hivyo*; nilijua kufanya hivyo ingemkasirisha Mungu na kuja chini ya laana.

*Nilikuwa nimeona ono; nilijua hivyo, na nilijua kwamba Mungu alijua hivyo, na singeweza kukana hivyo, na kudhubutu kafanya hivyo.*

Nilipata maamuzi akilini mwangu kuhusu madhehebu ya ulimwengu— sikuwa na haja kujiunga na lolote kati yao, bali kuendelea kama nilivyokuwa mpaka nipate maongozi zaidi. Nilikuwa nimepata ushuhuda wa Yakobo kuwa wa kweli— kwamba mtu akipungukiwa na hekima aombe dua kwa Mungu na atapokea na hatakemewa.

Niliendelea kufanya kazi zangu za kawaida katika maisha mpaka tarehe ishirini na moja Septemba, mwaka wa elfu moja mia nane na ishirini na tatu, wakati wote nikiteseka kwa udhalimu mkali sana mikononi mwa watu wa kila ngazi, wote watu wa dini na wasiokuwa wa dini, kwa sababu niliendelea kuthibitisha kwamba niliona ono.

Katika kipindi cha muda uliopita kati ya wakati nilipata ono lile na mwaka wa elfu moja mia nane na ishirini na tatu— nilikuwa nimekatazwa kujiunga na madhehebu ya kidini ya wakati huo na nikiwa wa umri mdogo sana na nikidhalimiwa na wale ambao wengefaa kuwa marafiki zangu na kunitendea mimi kwa ukarimu, na kama wangefikiria kuwa mimi, nimedanganyika wangefanya jitihada katika njia nzuri na njia ya mapenzi kuniongoza mimi— niliachwa kukabiliana na majaribio na kukutana na kila aina ya watu, mara nyingi niliingia kwenye makosa ya kipumbavu na kuonyesha udhaifu wa ujana na upungufu wa kibinadamu; ambao, mimi

najuta kusema, ulinielekeza kwenye majaribio tofauti tofauti, yanayochukiza machoni mwa Mungu. Nikifanya huu uugamo, hakuna hata mmoja anayefaa kufikiria mimi nina hatia ya dhambi au maovu makuu. Tabia ya kufanya mambo kama hayo haikuwa katika dhamira yangu.

## Matembezi ya Moroni

*Udhalimu uliendelea kadiri Joseph alikataa kukana kwamba alimuona Mungu. Siku ya 21 Septemba 1823 baada kuenda kitandani, Joseph aliomba ili aweze kujua msimamo wake mbele za Bwana. Malaika Moroni alimtokea.*

Jioni ya siku iliyotajwa tarehe ishirini na moja ya Septemba, baada kuenda kitandani changu kwa usiku ule, nilianza maombi na kufanya dua kwa Mwenyezi Mungu kwa msamaha wa dhambi zangu zote na matendo yangu ya upumbavu na pia kwa onyesho kwangu ili niweze kujua hali na msimamo wangu mbele zake; kwa sababu nilikuwa na matumaini zaidi juu ya kupokea ono takatifu, kama hapo awali.



*Miaka mitatu baadaye ya ono la kwanza la Joseph Smith, Mungu alimtuma malaika Moroni ili kumfunza Joseph kuhusu kurudishwa kwa Injili ya Yesu Kristo.*

Ningali nikiwa katika kitendo cha kumuomba Mungu, niligundua mwangaza ukitokea katika chumba changu ambao uliendelea kuongezeka mpaka chumba kikawa kimengaa zaidi ya mwangaza wa adhuhuri, wakati punde mtu alitokea kando ya kitanda changu, akisimama katika hewa, kwa vile miguu yake haikugusa sakafu.

Alikuwa amevalia joho lililolengea la weupe mwingi zaidi. Weupe wake ulikuwa zaidi ya chochote cha duniani ambacho nilikuwa nimewahi kuona; wala sifikirii kwamba chochote cha duniani kinaweza kufanywa kuonekana na weupe mwingi na uangavu mwingi. Mikono yake ilikuwa wazi na mikono yake pia, kidogo juu ya kiwiko; hata pia miguu ya ilikuwa wazi, pia miguu yake, kidogo juu ya visigino. Kichwa chake na shingo vilikuwa wazi. Niligundua kuwa hakuwa na nguo nyingine bali joho hili kwa vile lilikuwa wazi, hata kwamba ningeweza kuona kifua chake.


Sio tu joho lake lilikuwa jeupe zaidi lakini hata mwili wake wote ulikuwa na utukufu usio na kifani, na uso wake kama umeme. Chumba kilikuwa kimeangazwa zaidi, lakini sio vile uangazi zaidi uliomuzunguka mtu huyu. Nilipomtazama mara ya kwanza nilimwogopa; lakini uoga uliniancha mara moja.

Aliniita kwa jina langu na kuniambia kwamba alikuwa mjumbe aliyetumwa toka uwepo wa Mungu kuja kwangu na kuwa jina lake lilikuwa ni Moroni; kwamba Mungu anayo kazi anayotaka mimi nifanye na kwamba jina langu litachukuliwa kwa uzuri na ubaya kati ya mataifa yote, ukoo na ndimi au litasemwa kwa uzuri na kwa ubaya kwa watu wote.

Alisema kulikuwa na kitabu kilichofichwa, kilichoandikwa kwenye mababamba ya dhahabu, kinachopeana habari za watu wa kale wa bara hili, na chanzo cha kule walipotoka. Alisema pia kuwa ujalivu wa Injili ya milele ulikuwa ndani yake kama ulivyoletwa na Mwokozi kwa watu wa kale walioishi kwenye hilo bara.

Pia kulikuwa na mawe mawili katika upinde wa fedha— na mawe haya yamefungwa kwenye ngao ya kifuo inayofanyiza kile kinachoitwa Urimu na Thumimu— vimefichwa pamoja na mabamba; milki na utumizi wa mawe haya ndiyo uliofanyiza waoni wa kale au wa hapo awali na Mungu aliwatayarisha wao kwa madhumuni ya kutafsiri kitabu hiki.

Baada ya kuniambia mambo haya, alianza kumukulu unabii ulio katika Agano la Kale. Kwanza alitaja sehemu ya sura ya tatu



*Katika mwaka 421 nabii Moroni alifunika kwa ardhi maandishi matakatifu ya watu wake katika Kilima Cumorah. Akirudi baadaye kama kiumbe kilichofufuliwa, alimwambia Joseph Smith juu ya maandishi ya kale, ambayo ndani yake ilikuwemo injili jalivu kama ilivyo panawa na mwokozi kwa wakazi wa kale wa bara la Marekani. Maandishi haya ni Kitabu cha Momoni.*

ya Malaki; na pia akataja sehemu ya nne au sura ya mwisho ya ufunuo huu, ikiwa na mageuzi madogo kutokana na vile inavyosema katika Bibilia zetu. Badala ya kutaja mstari wa kwanza kama inavyosema katika vitabu vyetu, alitaja kwa jinsi hii:

"Kwani tazama, siku inakuja ambayo itachoma kama tanuu, na wale wale walio na majivuno, ndio na wale wote wanaofanya maovu watachomwa kama mabua; na wale wataokuja watawachoma asema Bwana wa Majeshi, kwamba hakutawachwa shina au tagaa."

Na tena akanukulu mstari wa tano unaosema; "Tazama nitakufunulia kwako ukuhani kwa mkono wa nabii Eliya kabla ya kuja kwa ile siku kuu na ya kuogofya ya Bwana."

Pia alitaja mstari ufuatao kwa njia nyingine: Na atapanda katika mioyo ya watoto maagano yaliyofanyiwa baba zao na mioyo ya watoto itawarudia baba zao. Na kama sio hivyo, dunia yote ingeangamia kabisa kabla kuja kwake."

Na zaidi ya haya, alitaja sura ya kumi na moja ya Isaya, na kusema uko karibu kutimizwa. Pia alitaja sura ya tatu ya Matendo ya Mitume, mstari wa lshirini na mbili na ishirini na tatu sawa kabisa kama vile inavyosema katika agano jipya letu. Alisema kwamba huyu nabii ni Kristo; lakini siku haijakuja ambapo "Wale ambao hawatasikia sauti yake watakatwa kutoka katikati ya watu," lakini karibuni itakuja.

Pia alitaja sura ya pili ya Yoeli, kutoka mstari wa ishirini na nane mpaka mwisho. Na pia akasema kwamba hii bado haijatimia, lakini karibuni itakuwa hivyo. Na akasema zaidi kwamba ujalivu wa Wayunani utakuja karibuni. Alitaja mafungu mengi ya maandiko matakatifu na kupeana maelezo mengi ambayo hayawezi kuelezwa hapa.

Tena aliniambia mimi, kwamba wakati nikipata haya mabamba ambayo amesema juu yake— kwa vile wakati ambao yatapatikana bado haujatimia— nisiyaonyeshe kwa mtu yeyote; hata pia ngao ya kifua pamoja na Urimu na Thumimu; ila tu wale ambao mtaamrisha kuwaonyesha na nikifanya kinyume nitaangamizwa. Na wakati alikuwa akizungumza nami juu ya mabamba, *ono lilifunguliwa kwenye akili zangu kwamba niliona mahali ambapo mabamba haya yalikuwa yamefichwa* na hata ikawa wazi na dhahiri kabisa, ili kwamba nilijua hapo mahali nilipopatembelea.

> *Ono lilifunguliwa kwenye akili Zangu kwamba niliona Mahali ambapo Mabamba haya Yalikuwa Yamefichwa*

Baada ya mawasiliano haya, niliona mwangaza katika chumba ukianza kukusanyika mara moja karibur na huyu mtu ambaye aikuwa akiongea nami, na ikaendelea kufanyika hivyo mpaka chumba kikawa giza tena, bali pale alipokuwa; wakati huo punde niliona kama kianga kikafunguka hadi mbinguni na akapaa mpaka akatokomea kabisa na chumba kikabaki vile kilivyokuwa kabla ya mwangaza wa mbinguni haujatokea.

Nilikaa nikifikiria juu ya tukio hili la kipekee, nikishangaa sana na yale niliyoambiwa na huyu mjumbe wa maajabu wakati nikiwa katikati ya fikira zangu, niligundua kwamba chumba changu kilianza kuangazwa tena na mara moja, kama vile ilivyokuwa yule yule mjumbe wa mbinguni alikuwa kando ya kitanda changu tena.

Alianza na mara nyingine kurudia mambo yale yale ambayo aliyofanya katika hili safari ya kwanza, bila ya kutofautiana hata kidogo; baada ya kufanya hivyo, alinijulisha mimi juu ya hukumu kuu ambayo ilikuwa inakuja juu ya ulimwengu, pamoja na ukiwa mkuu wa njaa, vita na maradhi ya kuambikizwa na kwamba huu hukumu mkali utakuja juu ya ulimwengu katika kizazi hiki. Baada ya kunieleza mambo haya, tena alipaa kama alivyokuwa amefanya hapo mapema.

Kufikia wakati huu, mawazo haya yalikuwa yameingia akilini mwangu kwa dhati, hata usingizi ulikuwa umetoroka kutoka machoni mwangu, na nikajilaza gharikika na mshangao juu ya kile nilichokiona na kusikia. Lakini cha kunishangaza tena nilimwona mjumbe yule yule kando ya kitanda changu, na nikamsikia akikariri au kurudia tena yale maneno kama ilipokuwa awali; na kuongezea onyo kwangu akiniambia mimi kwamba Shetani atajaribu kunijaribu mimi (kwa sababu ya hali ya ufukara wa familia ya baba yangu), kupata haya mabamba kwa ajili ya kujitajirisha. Haya alinikataza, akisema kwamba ni lazima nisiwe na nia ingine ya kupata haya mabamba ila kutukuza Mungu, na ni lazima nisishawishike na sababu yoyote nyingine bali tu ile ya kujenga ufalme wake; kama sivyo sitayapata.



*Kilima Cumorah ni kama kiasi cha maili tatu kusini-mashariki mwa shamba la Smith katika Palmyra, New York. Katika nyakati za Joseph pande ya kasikazini kulikuwa na nyasi, pande ya kusini kukawa na miti ya mbao na msitu. Mabamba yalikuwa yumefunikwa chini ya ardhi upande wa kusini magharibi, ambapo sio mbali kutota juu. Picha: Augusti 1907.*

Baada ya kuzuru mara tatu, tena alipaa na kuenda mbinguni kama hapo awali na mara nyingine niliwachwa nikiwaza juu jambo

lisilo la kawaida ambalo nililoliona; mara tu baada ya, mjumbe huyu wa mbinguni kupaa na kuniondokea ile mara ya tatu, jogoo akawika, na nikaona kwamba siku ilikuwa inaanza, kwa hivyo mazungumzo yalikuwa yamechukua usiku ule wote.



*Moroni alirudi mara moja kwa mwaka kwa miaka minne na kumfunza nabii kijana, baada ya hiyo miaka minne Joseph alipokea hayo mabamba na kuanza kutafsiri Kitabu cha Momoni.*

Muda mfupi baadaye niliamka kutoka kitandani mwangu, na kama kawaida, nikaenda kwenye shughuli zangu za kila siku; lakini nilipojaribu kufanya kazi kama nilivyofanya ule wakati mwingine, nilijipata kuwa nguvu zangu zimekwisha hata kunifanya mimi kuwa sijiwezi kabisa. Baba yangu, ambaye alikuwa akifanya kazi pamoja nami, aligundua kuliwa na kitu kilichukuwa siyo sawa nami, na akaniambia mimi niende nyumbani, nikaanza nikiwa na nia ya kuenda nyumbani; lakini katika jaribio la kuruka na nitoke kwenye shamba pale tulipokuwa, nguvu zangu ziliniishia kabisa, na nikanguka hoi kwenye mchanga, na kwa muda nikawa kabisa bila fahamu ya chochote.

Kitu cha kwanza ambacho naweza kukumbuka kilikuwa ni sauti ikinisemesha mimi, ikiniita kwa jina. Nikatazama juu, na kuona mjumbe yule yule amesimama juu ya kichwa changu, amezungukwa na mwangaza kama mbeleni. Akanieleza tena mambo ambayo alikuwa ameniambia usiku uliopita, na kuniamuru niende kwa baba yangu na kumueleza juu ya ono na amri ambazo nilikuwa nimepokea.

Nilitii; nikarudi kwa baba yangu kwenye shamba, na kumuelezea mambo yote. Alinijibu na kusema kwamba yalikuwa ya Mungu na akaniambia niende na kutenda kama nilivyoamriwa na huyo mjumbe. Niliondoka kutoka shambani, na kuenda mpaka pale mahali ambapo mjumbe alikuwa ameniambia kuwa mabamba yalikuwa yamefichwa; na kwa sababu ya uwazi wa ono hilo ambalo nilikuwa nimepata kuhusu juu yake, nilijua hapo mahali mara moja nilipofika hapo.

### Maandishi Matakatifu

Karibu na kijiji cha dia Manchester wilaya ya Ontario, New York, kuna kilima kikubwa na kilicho kikuu katika eneo lote. *Katika upande wa magharibi wa kilima hiki, sio mbali kutoka kilele, chini ya jiwe kubwa, palikuwa na mabamba yaliyofichwa kwenye sanduku la mawe*. Hili jiwe lilikuwa pana na duara katika upande wa juu na jebamba ukingoni ili kwamba sehemu ya kati ilikuwa inaweza kuonekana juu ya mchanga, lakini kingo zote zilikuwa zimefichwa na takataka.

Baada ya kuondoa takataka, nilipata mtaimbo ambao niliuingiza ndani ya ukingo wa lile jiwe na kwa kutumia nguvu kidogo liliinuka juu, Niliangalia ndani,na hapa kwa hakika niliona yale mabamba, Urimu na

Thumimu, bamba la kifua kama ilivyosemekana na mjumbe. Sanduku ambalo lilikuwa na vitu hivi lilikuwa ni kama mawe yaliyounganishwa na simiti. Chini ya sanduku kulikuwa na mawe mawili yaliyokaa pembe hadi pembe ya sanduku na juu ya mawe haya kuliwekelewa mabamba na vitu vingine vilivyokuwemo.

> *Katika upande wa Magharibi wa kilima hiki, sio mbali kutoka kilele, chini ya jiwe kubwa, palikuwa na mabamba yaliyofichwa kwenye sanduku la mawe.*

Nilijaribu kuvitoa nje, lakini nilikatazwa na mjumbe, na mara nyingine nilifahamishwa kwamba wakati wa kuvitoa mbele ulikuwa haujafika hata hautafika mpaka miaka minne kutoka wakati huo; lakini akaniambia kwamba nitakuja mahali hapo wakati kama huu kila mwaka na atakutana nami hapo na kuendelea kufanya hivyo mpaka utakapofika wa kupokea mabamba hayo.

Vivyo hivyo, kama nilivyoamrishwa, nilienda mwisho wa kila mwaka na kila wakati nilimpata mjumbe huyu huyu hapo na kupokea mafunzo na elimu kutoka kwake katika kila mazungumzo, kuhusiana na kile ambacho, Bwana atakachofanya na jinsi na kwa njia gani ufalme wake utaendoshwa katika siku za mwisho.

Kwa sababu hali ya baba yangu ilikuwa duni, ilitubidi kufanya kazi na mikono yetu kufanya vibarua au vingine kama vile tulivyopata kazi. Wakati mwingine tulikuwa nyumbani na wakati mwingine tukiwa mbali na kwa kuendelea na kazi kulituwezesha kupata maisha mema.

*Joseph alifanya kazi kadha na kupatia familia yake maisha mema. Katika mwaka wa 1825 alipata kazi katika wilaya Chenango, New York. Huko alikutana na Emma Hale, ambaye alimuoa tarche 18 Januari 1827.*


Mwishowe wakati ukafika wa kupokea mabamba ya Urimu na Thumimu na bamba ya kifua. Katika siku ya Ishirini na mbili ya Septemba mwaka wa elfu moja mia nane na ishirini na Saba, nilipoenda kama kawaida mwisho wa mwaka mwingine mahali ambapo yalikuwa yamefichwa, mjumbe wa mbinguni alinipatia mimi maagizo haya: kwamba kama ningeviachilia ovyo ovyo au kupitia kwa uzembe wangu, nitakatiliwa mbali; lakini kama nitafanya juhudi yangu yote kuvitunza, mpaka huyu mjumbe atapovihitaji, vitatakiwa kukingwa.

Punde nilipata kujua sababu gani nilipokea maagizo makali ya kuviweka salama na kwa nini mjumbe alikuwa amesema kwamba baada ya kufanya yote yaliyokuwa yanatakiwa juu yangu atavihitaji. Punde ilipojulikana kwamba nilikuwa navyo, kulitumiwa mbinu zote ili kuvichukua kutoka kwangu. Kila mpango ulibuniwa kwa madhumuni hayo. Udhalimu ulikuwa mkali na mabaya kushinda mbeleni na umati ulijitayarisha kila mara kuvichukua kutoka kwangu kama ingewezekana. Lakini kwa hekima ya Mungu, vilibakia salama mikononi mwangu, mpaka nilipokamiliza kile kilichokuwa kinahitajika mikononi mwangu. Wakati huyu, kama vile mpango ulinjokuwa, mjumbe alivihitaji tena, na nilimpatia; na yeye ndiye aliye navyo mpaka siku hii ikiwa siku ya pili ya Mei, elfu moja mia nane na thelathini na nane. . . .

Katika siku ya tano ya Aprili, 1829, Oliver Cowdery alikuja kwenye nyumba yangu, ambaye nilikuwa sijawahi kumuona. Aliniambia akiwa mwalimu katika shule iliyokuwa karibu na pale baba yangu alipoishi, na baba yangu akiwa mmoja wa wale waliopeleka watoto kwenye hiyo shule, alikuja kuishi naye kwa muda na alipokuwa hapo familia yangu ilimuelezea juu ya vile nilipokea mabamba, na basi hivyo akaja kuniuliza.

Siku mbili baada kuwasili kwa Bwana Cowdery (ikiwa tarehe 7 Aprili) nilianza kutafsiri kitabu cha Momoni, na akaanza kuniandikia.

*Katika mwezi Aprili ya 1829 Joseph Smith na Oliver Cowdery akiwa muandishi, alianza kutafsiri Kitabu cha Momoni kwa kipawa na uwezo wa Mungu. Baada ya Joseph Smith kumaliza, watu wengine walipata fursa ya kuona mabamba ya dhahabu mashahidi hawa wakaandika ushuhuda wao, kwa "vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno litathibitishwa" (2 Wakorintho 13:1).*



*Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho lilianzishwa katika nyumba ya Peter Whitmer Mkuu, tarehe 6 Aprili 1830. Karibu watu 60 walishuhudia kama vile ilivyohitajika na New York watu 6 kuanzisha kundi la kidini.*

## Ukuhani Ulirudisha

Tuliendelea na kazi kutafsiri, wakati, katika mwezi uliofuata (Mei, 1829), sisi katika siku fulani tulienda kwenye kichaka ili tuombe na kumuuliza Bwana juu ya ubatizo kwa msamaha wa dhambi, ambao tulikuwa tumeona umetajwa katika tafsiri ya mabamba. Wakati tulikuwa tunajishughulisha na kuomba na kumsihi Bwana, mjumbe kutoka mbinguni aliteremka katika wingu la mwanga, na kutuwekelea mikono, kututawaza, akisema:

"Juu yenu watumishi wenzangu, katika jina la masiya, ninawapatia Ukuhahi wa Haruni, ule ambao una funguo za huduma ya malaika na za injili ya toba, na za ubatizo kwa kutoza kwa msamaha wa dhambi; na huu hautatwaliwa tena kutoka ulimwenguni mpaka wana wa Lawi watafanya toleo tena la dhabihu kwa Bwana katika haki."

Alisema huu Ukuhani wa Haruni haukuwa na uwezo wa kuwekelea mikono kwa kipawa cha Roho Mtakatifu, bali kwamba huu utapeanwa kwetu baadaye, na akatuamuru sisi tuende na kubatizwa na kutupatia mwongozo kwamba mimi nimbatize Oliver Cowdery, na kwamba baadaye anibatize mimi.




*Joseph Smith na Oliver Cowdery walipokea Ukuhani wa Haruni kwa kuwekelewa mikono kutoke kwa Yohana Mbatizaji tarehe 15 Mei 1829.*

Vivyo hivyo tulienda na tukabatizwa. Nilimbatiza yeye kwanza na baadaye akanibatiza mimi— baada ya hapo nikamwekelea mikono juu ya kichwa chake na kumtawaza yeye katika Ukuhani wa Haruni na baadaye akaniwekelea mikono

yake juu yangu na kunitawaza kwenye Ukuhani huo huo— kwa vile tulivyoamriwa.

Mjumbe aliyetutembelea sisi wakati huu na kutupatia Ukuhani huu juu yetu, alisema kwamba jina lake likikuwa ni Yohana, huyo huyo ndiye anayeitwa Yohana mbatizaji katika Agano Jipya, na kwamba alitenda hivyo chini ya maongozi kutoka kwa Petro, Yakobo na Yohana, ambao walikuwa na funguo za Ukuhani wa Melchizedeki, ambao ni Ukuhani, alisema utapeanwa kwetu kwa majira yake na kwamba nitaitwa Mzee wa kwanza, wa Kanisa, na yeye (Oliver Cowdery) wa pili. Ilikuwa siku ya kumi na tano ya mwezi Mei, 1829, ambapo tulitawaza chini ya mkono ya mjumbe huyu na kubatizwa.



Punde tulipotoka kutoka majini baada ya kubatizwa, tulipokea baraka kuu na takatifu kutoka kwa Baba yetu wa Mbinguni. Nilipombatiza Oliver Cowdery, hapo roho mtakatifu akamushukia na alisimama na kutabiri mambo mengi ambayo karibuni yatakuja kupita. Na tena, mara tu nilipobatizwa na yeye, pia nilipata Roho wa unabii, wakati, nikisimama nikatabiri kuhusiana na kusitawi kwa kanisa, na mambo mengi yaliyohusikana na kanisa, na kizazi hiki cha watoto wa watu. Tulijazwa na Roho Mtakatifu na tukafurahia katika Mungu wa wokovu wetu.



*Kitabu cha Momoni, kwanza kilichapishwa mwaka 1830 na katika wakati huu kimechapishwa katika lugha zaidi ya 80 duniani kwote.*

*Huu ni ushuhuda wazi na wa haki wa Joseph Smith, akipeana mambo yaliyoleta kurudishwa kwa lnjili na kuanzishwa kwa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.*

*Kwa maelezo kamili juu ya hadithi ya Joseph Smith, tazama Historia— ya Joseph Smith, katika Lulu ya Thamani Kubwa* au Historia ya Kanisa, 1:2–79.